BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 03 Machi, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Mswada wa Kufuta Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nambari 1 ya Mwaka 2012 na Kutunga Upya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar na Kuweka Masharti Yanayohusika na Huduma za Miundombinu ya Tehama na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## III. MASWALI:

### Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

139. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Wananchi wa maeneo ya Kombeni na Maungani, jimbo la Dimani wamekuwa na changamoto ya kupata umeme mdogo kutokana na nguvu ndogo ya "transformer" iliyopo hospitali ya Kombeni, hali ambayo inaleta shida hasa kwa wajasiriamali wanaotegemea nishati ya umeme katika shughuli zao.

(a) Je, watendaji wa Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) wanafahamu uwepo wa changamoto hiyo.

(b) Je, hatua gani za haraka na dharura ambazo ZECO wamepanga kuzichukuwa ili kuwasaidia wananchi na wajasiriamali wa Kombeni na Maungani kuondokana na athari za umeme mdogo.

### Wizara ya Afya:

38. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na ongezeko kubwa la idadi ya watu wanaohudumiwa, Kituo cha Afya cha Pandani kimekuwa kidogo sana kukidhi haja ya uanzishwaji wake. Aidha, kituo hicho ni kibovu sana, chenye dari iliyoanguka na kuvuja kupita kiasi, huku kukiwa na wafanyakazi watatu tu wanaowahudumia wananchi wasiopungua 7,350.

Pamoja na kwamba wafanyakazi wa kituo hicho wenye stashahada (diploma) wamefanya kazi kwa zaidi ya miaka 30, inasikitisha kwamba marekebisho mapya ya mishahara imewaweka kwenye ngazi na kiwango cha malipo ya chini ukilinganisha na wafanyakazi wa vituo vyengine wenye astashahada (certificate) tu na wasio na umri mkubwa wa kazi.

(a) Je, kwa nini Serikali haikihudumii ipasavyo Kituo cha Afya cha Pandani na wafanyakazi wake.

(b) Je, ni vigezo vipi vimetumika na Serikali kuwapandisha wafanyakazi wenye astashahada (certificate) tu na wasio na umri mkubwa wa kazi na kuwateremsha wafanyakazi wenye stashahada (diploma) na umri mkubwa wa kazi.

(c) Je, ni upi mpango wa muda mfupi na wa muda mrefu wa Serikali wa kukifufua na kukitanua Kituo cha Afya cha Pandani.

118. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kituo cha Afya cha Kiembesamaki na Shakani vipo katika hali hatarishi kwa wagonjwa na wauguzi.

Je, ni ipi ahadi ya Serikali ya kuvikarabati vituo hivyo ili kuweza kutoa huduma nzuri na salama za kiafya kwa wananchi.

<u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

122. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Wanafunzi wa shehia ya Shakani na Buyu hufuata huduma ya elimu kwa masafa marefu, hali inayopelekea kuwepo changamoto tofauti ikiwemo masuala ya udhalilishaji na ufaulu mdogo.

Je, ni lini Serikali itajenga skuli ya msingi kwa ajili ya kuondosha changamoto za aina hiyo kwa wanafunzi na wazazi wa maeneo hayo.

153. MHESHIMIWA HABIB ALI MOHAMED (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa TASAF imetumia fedha nyingi kuiboresha skuli ya Piki Msingi na Sekondari na kwa sasa skuli hiyo iko katika hali nzuri na ina madarasa ya kutosha.

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha darasa la kumi na tatu (13) na kumi na nne (14), hasa ukizingatia kuwa masafa baina ya Wete, Piki na Chake Chake ni makubwa.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

56. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Michezo ni moja ya burudani kwa watu wengi duniani, pia imegeuka kuwa moja ya vyanzo vya ajira vyenye kuleta mapato kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa fursa nyingi za kimichezo, bado Serikali yetu haijazitumia fursa hizo vyema wala kuweka mpango mkakati imara wenye nia ya kuinua michezo nchini.

(a) Je, Serikali ina utaratibu gani wa kuandaa mitaala ya

mafunzo kwa viongozi wa vyama vya michezo, ili kuwawezesha kusimamia na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi, uweledi na uwazi.

(b) Je, Serikali imefikia wapi katika suala la Zanzibar kujiunga na kujitegemea katika mashirika ya michezo ya kimataifa kama vile FIFA, ili kuviwezesha vyama vyetu kushiriki na kujitangaza kimataifa.

(c) Je, Serikali imefikia wapi katika kuanzisha viwanja vya michezo vya Wilaya (4-in-1).

68. MHESHIMIWA SALMA MUSSA BILAL (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Imekuwa ni jambo la kawaida kwa vituo vyetu vya ZBC upande wa Televisheni kurusha vipindi ambavyo vinakosa mvuto kutokana na kosa la kuruka kwa vipindi hivyo pamoja na kuvirejea sana kama kwamba Zanzibar haiwezi kupata vipindi bora zaidi vitakavyohamasisha wananchi kuviangalia na kuvipa mgongo vipindi vya vituo vyengine vya nje ya Zanzibar.

(a) Kwa nini hadi leo Serikali imekosa wahisani wa kukifadhili kituo hicho.

(b) Je, imefikia wapi mipango ya kuwawezesha kielimu wafanyakazi wazalendo ambao watatayarisha vipindi kiueledi.

(c) Kwa nini hadi sasa hatuna vipindi endelevu kama michezo inayotafsiriwa kwa lugha yetu ambayo inachezwa nchi nyengine ukiachia mbali ile ya wachina.

<u>**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**</u>

46. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na jitihada kubwa za makampuni ya simu katika kuleta huduma za simu za mkononi hapa nchini, bado kuna maeneo mengi Zanzibar, ambapo huduma hii imekuwa adimu au isiyo ya uhakika:

(a) Je, ni ipi hali halisi (status) ya upatikanaji wa huduma ya mitandao ya simu za mkononi (coverage) kwa Zanzibar.

(b) Je, ni lini Serikali imeyaelekeza makampuni ya simu za

mkononi yanayowekeza Zanzibar kukamilisha mitandao yao ili kuwafikia wananchi wote wa Zanzibar mijini na vijijini.

(c) Je, umefikia wapi mpango wa kuviwezesha vitengo vya kibiashara vya kiserikali kutumia Mkonga hadi kwenye Nyumba “Fiber to the Home (FTTH)”.

164. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwepo na msongomano mkubwa bandarini Malindi hasa pale meli zinapotoka Pemba au zinapofunga gati, boti au meli mbili kwa wakati mmoja. Hali ambayo inapelekea usumbufu mkubwa kwa abiria na pia kukosekana umakini katika ukaguzi wa abiria na mizigo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kulitatua jambo hili kwa haraka ili tuepushe kuja kutokezea madhara na pia kuwafanya wananchi kusafiri bila usumbufu wowote.

(b) Je, Wizara inasemaje kuhusiana na kuwepo kwa maegesho ya kutosha bandarini hapo, ili kukwepa usumbufu uliopo.

168. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa zoezi la uwekaji namba katika nyumba lilifanyika vizuri na kupiga hatua nzuri wakati wa maandalizi ya sensa. Na kwa kuwa zoezi hili limesita kwa sasa na linaonekana kama kwamba limeisha wakati zipo nyumba ambazo wamiliki wake wamelipa, lakini hawajawekewa namba na hakuonekani hamasa na muendelezo wa zoezi hili. Na kwa kuwa zoezi hili ni muhimu kwa ajili ya utambuzi wa anuani za nyumba na majengo yetu na kuweza kutumika kwa njia mbali mbali kama vile huduma za posta na biashara za mtandaoni.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha zoezi hili linakuwa endelevu na kuleta tija iliyokusudiwa.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

161. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Zanzibar tumekuwa tukipokea miongo tofauti ya mvua licha ya kupotea kwa utaratibu tuliouzoea wa mvua hizo, kutokana na mabadiliko ya tabia nchi.

(a) Ni lini Serikali itavuna na kuyahifadhi maji ya mvua, ili yaweze kutumika katika shughuli mbali mbali za mzunguko wa maisha yetu.

(b) Ni changamoto gani zinazopelekea kukwamisha mpango huu na matokeo yake tunayaacha maji ya mvua kupotea na kutuama maeneo sio sahihi kwa matumizi.

(c) Je, mpango huu wa kuvuna maji ya mvua unaweza ukawa na faida katika Mfumo wa Umwagiliaji Maji (irrigation system).

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Mswada wa Kufuta Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar Nambari 1 ya Mwaka 2012 na Kutunga Upya Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Shirika la Mawasiliano Zanzibar na Kuweka Masharti Yanayohusika na Huduma za Miundombinu ya Tehama na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa mara ya Kwanza.

Zanzibar,
03 Machi, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.